

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MtwARA - MIKINDANI



TAARIFA KWA UMMA.

MAPOKEZI YA FEDHA MIL. 420 ZA UJENZI WA MADARASA YA SEKONDARI.

TAREHE 30/09/2022, MtwARA.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani COL. Emanuel Mwaigobeko anapenda kuutaarifu umma kuwa Ofisi yake imepokea fedha **Shilingi milioni mia nne ishirini tu** (420,000,000) kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **ishirini na moja (21)** vya Sekondari ikiwa ni maandalizi ya kupokea wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2023.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani imeshaanza kufanya maandalizi ya ujenzi wa madarasa hayo ili kuweza kuyakamilisha kwa wakati huku ujenzi wa darasa moja ukigharimu **Shilingi milioni ishirini tu** (20,000,000).

Imetolewa na:

Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

